# Kuna umuhimu wa Serikali kupunguza gharama za kufanya biashara nchini



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Godfrey Simbeye akihutubia wakati wa kongamano la majadiliano kuhusu changamoto za huduma za fedha kuwafikia wajasiriamali wadogo na wa kati nchini (Picha ya Tanzania Today).

Taasisi mbalimbali katika sekta binafsi nchini Tanzania zimekuwa zikilalamika kuwa mazingira ya biashara si rafiki kutokana na kuwapo kwa sheria zinazokwamisha biashara, ajira na uendeshaji wa ujasiriamali. Waajiri wanataka sehemu kubwa ya sheria za kazi kuangaliwa upya ili ziendane na mahitaji halisi ya biashara kwa sasa

Shirikisho la Waajiri nchini (ATE) linaitaka Serikali ya Awamu ya Tano kuangalia masuala ya sera na sheria zinazosababisha ufanyaji biashara nchini Tanzania kuwa ghali.

Linashauri kuwapo na majadiliano ya wazi ili kufikia makubaliano yatakayoondoa vikwazo vinavyokwamisha ustawi wa biashara nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Dk Aggrey Mlimuka anasema kwamba uendeshaji wa biashara nchini Tanzania unaweza kuwa bora na wenye ufanisi mkubwa kama baadhi ya sheria za kazi (miongoni mwa sheria na sera ambazo ni vikwazo) zitaangaliwa upya kwa kusikiliza hoja za waajiri na hivyo kuongeza wigo wa ajira na uendeshaji wa biashara.

Mtendaji huyo wa ATE anasema ni vyema vifungu vya sheria ambavyo si rafiki katika kazi kama mikataba ya ajira, muda wa kazi, kanuni za kuachishana kazi au kufukuzana, fidia kwa kuondolewa kazini bila taratibu, sheria kali na kanuni zinazogusa ajira kwa watu wasiokuwa watanzania, kuangaliwa upya na kuondolewa.

Dk Mlimuka anasema kwamba sera, sheria na kanuni ni lazima zitengeneze mazingira yenye mizania sawa inayokubalika na pande zote zinazohusika katika hali ya kiuhalisia. “Sheria za kazi pamoja na uzuri wake katika kudhibiti masuala ya kazi, zisivuruge waajiri na kudumaza ukuaji wa biashara,” anasema. Mtendaji huyo anaitaka Serikali kufanyakazi na ATE kuangalia athari za sheria, kanuni na mazingira ya biashara ili kuhakikisha kwamba waajiri wanakuwa na nafasi ya kukuza soko la ajira, huku wakitatua matatizo yanayokwamisha ukuaji wake.

Anasema kwamba sheria za kazi zina athari kubwa chanya na hasi katika ukuaji wa biashara na soko la ajira na ATE itaendelea kufanya utafiti, kufanya majadiliano na kutengeneza mifumo ya namna bora ya uendeshaji na uwezeshaji wa ajira nchini. Taasisi mbalimbali katika sekta binafsi nchini Tanzania zimekuwa zikilalamika kuwa mazingira ya biashara siyo rafiki kutokana na kuwapo kwa sheria mbalimbali zinazodhibiti ufanyaji biashara, ajira na uendeshaji wa ujasiriamali.

Pamoja na vikwazo hivyo sekta binafsi nchini Tanzania ndiyo inayotoa ajira kwa kundi kubwa la watu na ukuaji wake ni kitu muhimu kwa ajili ya kuzalisha ajira na kuimarika kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Dk Mlimuka, waajiri wanataka sehemu kubwa ya sheria za kazi kuangaliwa upya ili ziendane na mahitaji halisi ya biashara kwa sasa.

Baadhi ya sheria ambazo ATE inataka zifanyiwe mabadiliko kwa kuwapo awali kwa mazungumza kati yao na Serikali ili zipelekwe bungeni kufanyiwa mabadiliko ya kisheria na Bunge na hivyo kutoa mazingira bora ya kikazi kwa sekta binafsi na umma ni pamoja na:


1. Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi – Waajiri hutakiwa kuchangia asilimia moja ya malipo yao kwa wafanyakazi. Sheria hii inatumika huku baadhi ya taasisi zikiwa zimewakatia bima ya uhakika ya matibabu wafanyakazi wao. Waajiri wa aina hiyo wanaona Mfuko huu ni ongezeko la gharama katika uendeshaji wa shughuli zao.

2. Sheria ya kazi kwa wasiokuwa raia wa Tanzania. Waajiri wangelipenda kuona kwamba suala hilo linafikia mwisho kwa manufaa ya ukuaji wa ajira.

3. Sheria za kazi zinatakiwa kutoa mwongozo ulio wazi wa muda kwa wanawake wenye watoto wachanga kuondoka eneo la kazi na kwenda kunyonyesha. Sheria iko wazi kuhusu likizo ya uzazi lakini haikutoa maelezo ya wazi kuhusu kipengele cha unyonyeshaji.

4. Waajiri wangelipenda kuona sheria za kazi na uhamiaji zenye wastani kuhusu wafanyakazi wa kigeni hasa kutokana na kukosekana kwa Watanzania wenye utaalamu katika kazi za kitaalamu na zisizohitaji utaalamu. Kwa mujibu wa Dk Mlimuka kinachotakiwa ni kuwa na wafanyakazi wengi wenye uzalendo kwa taifa, wakati nchi inapambana na mfumo wake wa elimu ili kuwezesha kutoa wafanyakazi wanaotakiwa katika soko la ajira la kuzingatia matarajio ya waajiri.

5. ATE pia wanataka Sheria ya NSSF kufanyiwa mabadiliko. Kwa mujibu wa ATE, waajiri wanapata changamoto kubwa katika kufanya hesabu za michango ya wafanyakazi wao. “ Waajiri wanalazimia kukata asilimia 5 au 10 katika mshahara kwa kutegemea mkataba wa kazi. Hali hiyo imeanza tangu sheria ya hifadhi kufanyiwa mabadiliko mwaka 2012 (Namba 5 ya 2012).


Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Dk Aggrey Mlimuka

Utafiti uliofanywa na Shirika la Kazi Duniani (ILO) , uliangalia sheria za kazi, mazingira ya biashara na ukuaji wa biashara ndogo, uliionyesha kwamba baadhi ya sheria za kazi na kanuni zake ni kikwazo kwa ukuaji wa sekta. Sheria hizo zilisababisha ama biashara hizo ziendelee kuwa ndogo au kutosajiliwa. Kwa mujibu wa ATE, sheria za kazi zilizopo nchini ni moja ya sababu ya watu wengi kutosajili biashara zao. Hata hivyo, wamesema ni vyema utafiti wa kina ukafanyika ili kujua zaidi kiwango na namna ya kutanzua shida hiyo.

Dk Wilbert Kapinga kutoka kampuni ya wanasheria ya Mkono & Co anasema: “Tanzania ilibadili sheria zake za kazi mwaka 2004 wakati ilipopitisha Sheria ya Kazi na Mahusiano Kazini, sheria namba 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisi za Kazi, sheria namba 7 ya mwaka 2004. Wakati Sheria ya Kazi inaonyesha viwango vya kazi, Haki na wajibu; sheria ya taasisi za kazi inaonyesha taasisi zinazoshughulikia utekelezaji wa sheria za kazi.

**Jambo la kuzingatia**

Mazingira ya biashara ni mkusanyiko wa masuala yote ambayo yanatakiwa katika uendeshaji wa biashara. Mambo hayo ni pamoja na msukumo wa nje, taasisi na sheria na masuala mengine ambayo hayamo katika mipango ya mfanyabiashara lakini yanaathiri uendeshaji wa biashara kwa namna chanya au hasi- Mhariri

***Kwa maoni tuma katika mfumo wa ujumbe mfupi kwenda 0786240172. Utuambie unafikiria kifanyike nini kuboresha mazingira ya biashara nchini. Maoni yako ni muhimu kwetu na tunayaheshimu. Kutakuwa na kifuta jasho cha Sh30,000 kama muda wa maongezi kwa kila ujumbe utakaochapishwa.***

**SAUTI ZA WANANCHI**

**Michael Paul, Mwanafunzi wa MBA, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (Sua):**

Kodi na ushuru mbalimbali ni miongoni mwa mambo makubwa yanakwamisha biashara. Serikali mpya ya awamu ya tano inapaswa kuondoa vikwazo hivyo na kuondoa kodi zinazosumbua wafanyabiashara katika kukuza mitaji yao. Pia, kiwango cha riba kipunguzwe ili iwe rahisi kwa wajasiriamali kujiingiza katika biashara kwa njia ya kupata mkopo nafuu.

**Godson Elias, Mbeya:**

Shilingi ya Tanzania imekuwa ikipanda na kushuka. Kuna haja ya kuchukua hatua za makusudi kama nchi kuzalisha bidhaa zenye ongezeko la thamani badala ya kutegemea bidhaa za asili. Pia, muda umefika kwa serikali kufikiria kutoa ruzuku kwa kilimo na viwanda na kuongeza kodi kw abidhaa zinazotoka nje kwa lengo la kuhami viwanda vya Tanzania.

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA
BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo